**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA**

COSOTA
OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

# TANGAZO

## KUTAMBULISHWA KWA KAMPUNI ZA KUKUSANYA NA KUGAWA MIRABAHA KWA MWAKA 2025/2026: "SOCIETY OF MUSIC ADVOCACY LIMITED (SOMA)" NA "TANZANIA REPRODUCTION RIGHTS SOCIETY LIMITED (TANRRS)", KWA AJILI YA UTOAJI LESENI KUTOKANA NA MATUMIZI YA KAZI ZA MUZIKI NA MAANDISHI KATIKA MAENEO YA BIASHARA

**Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA)** inapenda kuutaarifu umma kuwa, kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999 kupitia **Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022** pamoja na **Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (**Kampuni za Ukusanyaji na Ugawaji Mirabaha)**, 2023** zilizotangazwa katika **Tangazo la Serikali Na. 211 na 215 la tarehe 24 Machi, 2023**, COSOTA ilitoa leseni za ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha tarehe **23 na 24 Julai, 2025**.

Leseni hizo zilitolewa kwa Kampuni ya **Society of Music Advocacy Limited (SOMA)** kwa ajili ya wabunifu wa kazi za muziki, na Kampuni ya **Tanzania Reproduction Rights Society Limited (TANRRS)** kwa ajili ya wabunifu wa kazi za maandishi. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa mabadiliko ya sheria yanayoruhusu makampuni binafsi yaliyoanzishwa na wasanii, waandishi, na wabunifu kushiriki moja kwa moja katika ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa mujibu wa Sheria ya hakimiliki na hakishiriki.

Hivyo basi, jukumu la kukusanya na kugawa mirabaha kwa kazi za muziki litatekelezwa na **Kampuni ya Society of Music Advocacy Limited (SOMA)** kwa kipindi kinachoanza tarehe **1 Julai, 2025** hadi **30 Juni, 2026**. Vilevile, **Kampuni ya Tanzania Reproduction Rights Society Limited (TANRRS)** itakuwa na jukumu la kukusanya na kugawa mirabaha kwa matumizi ya kazi za maandishi kwa kipindi hicho hicho, kuanzia **1 Julai, 2025** hadi **30 Juni, 2026**. Kutokana na mabadiliko hayo, COSOTA imebaki na jukumu la Usimamizi wa Kampuni hizo za ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha pamoja na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Kifungu cha 51 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2023.

Wadau wote wanaohusika kutakiwa kulipia leseni, watoe ushirikiano kwa Kampuni hizo ili wabunifu waendelee kupokea mirabaha na kunufaika na matumizi ya kazi zao. Viwango husika vya makusanyo na ugawaji wa mirabaha vitaandaliwa na SOMA na TANRRS na kuidhinishwa na COSOTA kwa ajili ya kuanza kutumika.

Wito kwa wasanii, watayarishaji na wabunifu wote ni kuhakikisha wanajiunga na Kampuni za Madaraja ya Kazi zao ili kuweza kunufaika zaidi na matumizi ya kazi zao. Taarifa zaidi kuhusu namna ya kujiunga na Kampuni hizo zinapatikana kupitia Kampuni hizo au kupitia Shirikisho la Muziki na Maandishi na Vyama vyake.

**Imetolewa na:**
**Ofisi ya Hakimiliki Tanzania – COSOTA**
**28 Julai, 2025**